**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. ASHATU KACHWAMBA KIJAJI WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MILIKI UBUNIFU DUNIANI, TAREHE 28 APRILI 2023**

**KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA JULIUS NYERERE (JNICC)**

**DAR ES SALAAM**

Prof. Neema Mori, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA),

Bw. Godfrey Nyaisa, Afisa Mtendaji Mkuu, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA),

Wakuu wa Taasisi zinazosimamia Miliki Ubunifu Tanzania Bara na Zanzibar,

Wakuu wa Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi mliyopo hapa,

Wabunifu na Wajasiriamali,

Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa BRELA,

Wageni Waalikwa,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Awali ya yote na kwa unyenyekevu mkubwa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo katika siku hii adhimu ya Maadhimisho ya Siku ya Miliki Ubunifu Duniani (W*orld Intellectual Property Day*).

Kwa namna ya kipekee niwashukuru BRELA kwa kuandaa maadhimisho haya ya Siku ya Miliki Ubunifu yanayoadhimishwa duniani kote kwa namna tofauti tofauti. Aidha, naomba kutambua uwepo wa Taasisi mbalimbali kama vile Ofisi ya Hakimiliki (COSOTA), Ofisi ya Hakimiliki Zanzibar (COSOZA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA), pamoja Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu za Mimea kwa jushirikiana na BRELA hutekeleza jukumu la kusimamia masuala ya Miliki Ubunifu Tanzania Bara na Zanzibar katika maeneo mahsus ya Miliki Ubunifu.

Nimefarijika sana kwa namna ambavyo maadhimisho haya yameandaliwa mwaka huu kwa kushirikisha Wajasiriamali na Wabunifu, hususan Wanawake kutoka sekta tofauti tofauti kwa kuzingatia Kauli Mbiu ya Siku ya Miliki Ubunifu Duniani kwa mwaka huu ambayo ni **"Wanawake na Miliki Ubunifu: Kuongeza Kasi ya Ubunifu katika Biashara"** kwa lugha ya kigeni, **"Women and IP: Accelerating Innovation and Creativity in Business."**

**Ndugu Washiriki**

Nimepata fursa ya kutembelea na kujionea bidhaa za wabunifu na wajasiriamali wote kabla sijaingia hapa ukumbini, nimefurahi kuona bidhaa na huduma zenye ubora na zilizotumia Miliki Ubunifu. Bidhaa na huduma hizi ni kiashiria tosha kuwa bidhaa na huduma zetu zinaweza kushindana Kikanda na Kimataifa kwa kuvuka mipaka ya Tanzania. Nawapongeza sana Wajasiriamali wote waliofanikiwa kuonesha bidhaa pamoja na huduma zao leo. Ni matumaini yangu kwamba kwa miaka inayokuja, Maadhimisho haya yatachukua sura ya Kitaifa na

yatajumuisha idadi kubwa zaidi ya Wabunifu ili kuwatambua na kuwaenzi watu hawa muhimu katika maendeleo ya Taifa letu.

**Ndugu washiriki**

Nimetaarifiwa kuwa asubuhi ya leo katika maadhimisho haya kumekuwa na mijadala mbalimbali kuhusu masuala ya Miliki Ubunifu, jambo zuri zaidi ni kwamba mijadala hiyo imehusisha wataalam na wadau mbalimbali katika sekta za umma na sekta binafsi. Kunapokuwa na ushirikishwaji wa sekta binafsi ambao ni waendesha uchumi wa nchi katika shughuli za kiserikali na mijadala mbali mbali, mara nyingi kunakuwa na uhalisia wa mijadala husika ambapo pande zote mbili yaani Sekta ya Umma na Binafsi zinakuwa na uelewa wa pamoja katika kutambua mafanikio na kubaini changamoto wanazokutana nazo wafanyabiashara hasa wajasiriamali. ***Hongereni sana.***

Nitoe rai kwa Taasisi za Serikali zilizopo hapa tukianza na Mhimili wa Mahakama, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), BRELA, BPRA, COSOTA, COSOZA, Tume ya Ushindani (FCC) na wengine kuhakikisha majadiliano mliyofanya leo yanawekewa mikakati ya namna bora ya kutatua changamoto zilizoibuliwa na wabunifu na wajasariamali katika majadiliano hayo. Hii itawawezesha kufanya kazi zao kwa mujibu wa Sheria na kwa kujiamini zaidi hasa katika zama hizi za maendeleo ya sayansi na teknolojia wakitambua kwamba Serikali inawathamini na kuhakikisha wanaongeza kasi ya Ubunifu katika kuendeleza bunifu na kukuza Biashara zao.

**Ndugu washiriki**

Serikali chini ya uongozi mahili wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kutekeleza Mikakati mbalimbali hususan utekelezaji wa malengo ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (*Blueprint)* ili kuweka mazingira bora na wezeshi kwenye sekta zote ikiwa ni pamoja na eneo la Miliki Ubunifu ambalo linakuwa kwa kasi duniani. Kwa sasa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuwepo kwa Sera ya Taifa ya Miliki Ubunifu (National Intellectual Property Policy). Ni matumaini yangu kuwa kukamilika kwa Sera hii kutasaidia kutoa miongozo itakayo imarisha miundo ya kisheria na kitaasisi katika eneo la Miliki Ubunifu, kuwa na taratibu rahisi na wezeshi za sajili na linzi mbalimbali, kuimarisha linzi zaidi na kuongeza maeneo mapya ya ulinzi wa Miliki Ubunifu. Maandalizi ya Sera hii yalihusisha Sekta ya Umma na Binafsi.

**Ndugu washiriki**

Kwa kuwa baadhi ya Sheria za Miliki Ubunifu ni za muda mrefu na kuna baadhi ya maeneo mengine bado hayalindwi kisheria, Serikali imeanza mchakato wa kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali za Miliki Ubunifu kwa lengo la kuziboresha ili ziweze kwenda na wakati na kutoa urahisi wa usamamiaji na uratibu wa Miliki Ubunifu nchini. Mchakato huu utakapo kamiliki usimamizi wa masuala ya Miliki Ubunifu utakuwa rafiki na wezeshi kwa wafanyabiashara kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwa ujumla. Nafahamu kwamba Sheria nyingine za usimamizi na utekelezaji wa Haki za Miliki Ubunifu zimeendelea kufanyiwa maboresho ili kuzifanya ziendane na mabadiliko mbali mbali ya kimazingira na kiteknolojia duniani.

Pamoja na Serikali kuhakikisha kunakuwa na Sera ya Taifa na Miliki Ubunifu na kufanya maboresho ya Sheria sheria za Miliki Ubunifu ili ziwe bora, nitoe rai kwa wananchi wote kutumia fursa zilizopo na zitakazoboreshwa kupitia marejeo ya sheria za Miliki Ubunifu ili muweze kunufaika na fursa hizi zinazotokana na matumizi ya Miliki Ubunifu kwa maendeleo yenu binafsi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Serikali inategemea kupitia Sera, Sheria na Programu mbalimbali zinazolenga kukuza na kuendeleza Miliki Ubunifu, changamoto mbalimbali katika jamii zitatatuliwa kutokana na bunifu zenu, sajili na linzi zitaongezeka ili kuepusha ukiukwaji wa matumizi ya Haki Miliki Ubunifu na mwisho bunifu hizi zitaleta faida kwa njia ya kuziuza au kutoa leseni za matumizi kwa kuwa zinapokuwa zimelindwa zinakuwa na hadhi kama mali nyingine, hivyo zitawezesha kuongezeka kwa pato la mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla, kama nilivyotangulia kusema awali.

**Ndugu washiriki**

Kupitia jukwaa hili ni vema tukawa na uelewa wa pamoja kuwa dunia ya sasa inalenga zaidi ukuaji na matumizi ya Ubunifu, Sayansi na Teknolojia, hivyo unapozungumzia Miliki Ubunifu unazungumzia Ubunifu, Sayansi na Teknolojia kama nguzo muhimu ya ukuaji wa uchumi, pasipo kutumia Miliki Ubunifu, ukuaji wa uchumi wa Taifa lolote utayumba sana. Kuna mifano mingi hai ya nchi nyingi zilizoendelea na zimepata mafaniki makubwa ya kiuchumi kupitia Miliki Ubunifu kama vile nchi za Magharibi na Asia.

Natambua BRELA wameweka mikakati mizuri ya kuboresha huduma wanazotoa na kusimamia kuvutia zaidi wabunifu wa kazi mbalimbali ili kuongeza idadi ya sajili na linzi za kazi zao pamoja na kuhakikisha wabunifu hao wanapata manufaa

ya kazi zao. Mikakati hiyo pamoja na uanzishaji wa maadhimisho haya, mashindano na Tuzo za Miliki Ubunifu nchini ambayo yanatategemewa kuanza katika siku za karibuni, kushirikiana na kutembelea wadau wa Miliki Ubunifu kama vile Taasisi na Vyuo pamoja na shule ili kutoa elimu ya Hataza na masuala mengine ya Miliki Ubunifu. Lengo la haya yote ni kuhakikisha kuwa Miliki Ubunifu inatumika kama chachu ya ukuaji wa uchumi wa mtu binafsi na Taifa kwa ujumla kutokana na umuhimu wake katika maendeleo. Hivyo, nawaasa wadau wote wa Miliki Ubunifu muongeze kasi ya khamasisha Ubunifu na utumiaji wa Miliki Ubunifu ili kuiwezesha nchi yetu kuwa katika nafasi nzuri ya matumizi ya teknolojia na ubunifu kwa maendeleo endelevu.

**Ndugu washiriki**

Kwa kumalizia naomba niwashurukuru sana washiriki wote hasa Wajasiriamali na Wabunifu walioshiriki pamoja na kuonesha bidhaa na huduma zao, Serikali itaendelea kuwasaidia kwa kuweka mazingira bora ya kukuza Ubunifu na ufanyaji biashara nchini ili msipate vikwazo vyovyote katika shughuli zenu. Vile vile, elimu iliyotolewa kupitia mada mbalimbali zilizojadiliwa leo iwe chachu ya kuimarisha matumizi ya Miliki Ubunifu katika kuongeza ubora wa bidhaa na mnyororo wa thamani.

**Mwisho**,

Nawapongeza wabunifu wote watakaopata Tuzo leo, tuzo hizi zikawe chachu ya kukuza Ubunifu katika Biashara ili wengine waone umuhimu wa kuendeleza na kukuza Ubunifu katika shughuli za kibiashara na Maisha ya kila siku!

**Asante sana kwa kunisikiliza.**